

# Pambazuko

Toleo Namba 0047

Jumatatu Septemba 18-24, 2023

## Tuhuma Nzito ... Akaunti ya IGP yadaiwa kulipwa mabilioni

*Ilikuwa ikiingiziwa Sh. 20,000 kwa kila saa; kwa kila siku – saa 12, ikiwamo Jumamosi, Jumapili na hata siku za sikukuu kwa kipindi cha mwaka mmoja.*

*Askari wanaolinda kwenye maeneo ya biashara binafsi; kwa makubaliano maalum, hulipwa kati ya Sh. 20,000 na 30,000 kwa kufanya kazi kwa saa 12.*



*Uk.16&17*

● *Yadaiwa kuingiziwa Sh. milioni 21 kila mwezi*

**Ikulu  
yatonywa,  
yachukua  
hatua haraka**  
Uk.5

**Mchengerwa  
azibe matobo  
Tamisemi**

**Uk.  
9**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

## Ahadi kuboresha bandari ni msingi

**K**AULI ya Rais wa Jamhuri Kya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwamba serikali itaendelea kutoa fedha ili kuboresha na kuimarisha miundombinu ya bandari zote, haiwezi kupita bila kupongezwa na wazalendo na wapenda maendeleo.

Maneno ya kiongozi huyo wa nchi, ni zaidi ya amri kwa maana kwamba sasa amewaagiza wasaidizi wake, kuendelea kujipanga kuhakikisha mafungu ya kuboresha na kuimarisha bandari zetu, yanapatikana na kutengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Rais Samia anatoa kauli hiyo akiwa ziarani Mtwara wiki iliyopita, lakini amekuwa akiirejea mara kwa mara, kuonyesha msisitizo wa matamano yake na Watanzania.

Kiongozi huyo wa Tanzania, anatambua umuhimu wa kuwa na bandari kubwa, zenye miundombinu ya kisasa ili kuleta ufanisi na hatimaye kuwepo kwa idadi kubwa ya shehena inayopakwa na kupakuliwa kupitia huko.

Tafsiri rahisi kuwepo idadi kubwa ya mizigo inayohudumiwa na bandari zetu, ni kupatikana kwa fedha nyingi zinazokusanywa na mamlaka kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania na watu wake.

Umuhimu wa kuwa na bandari zinazofanya kazi kwa ufanisi, kuwa na watendaji weledi wa wanaozingatia miiko yao ya kazi, unashuhudiwa na Rais Samia, na ndiyo maana anakuwa na uthubutu wa kutamka kwamba “anaongeza fedha zaidi ili kuziboresha bandari.”

Endapo bandari zetu zingekuwa

na “mchwa,” kwanza Rais Samia angesita kuelekeza kuongezwa kwa mafungu ya fedha ili kuziboresha, na zaidi sana angetumia mamlaka yake kupangua watendaji hao, ili kuhakikisha matamano yake yanafikiwa.

Ni kwa kauli hizo za Rais Samia, hivi sasa bandari karibu zote za Tanzania ama zinaendelea kupokea fedha za kuboresha miundombinu, ama ziko katika hatua kadhaa za kupokea fedha kwa ajili ya shughuli hiihiyo.

Sisi katika Pambazuko, pamoja na kuendelea kumpongeza Rais Samia kwa kuongeza mafungu ya fedha kuboresha bandari, pia hatuoni aibu kupongeza watendaji wa bandari zetu, wakiongozwa na Plasduce Mbossa.

Mbossa pamoja na timu yake ya watendaji; wa juu, kati na hadi kada ya chini, wameonyesha mfano wa kazi nzuri na kusimamia utekelezaji wa majukumu yao, hivyo Rais Samia kuendelea kuwa na imani nao.

Tunaamini kwamba usimamizi mzuri wa majukumu yao bandarini, kutachochewa zaidi kwa kuwepo miundombinu imara, bora na yenye usasa katika kuleta ufanisi zaidi wa bandari, hivyo kujihakikishia mapato zaidi.

Maana ya kuwa na mapato makubwa, kutatafsirika zaidi kwa kuona Tanzania inakuwa na shule bora, walimu wa kutosha, hospitali nyingi na bora zaidi, barabara zenye viwango, na zaidi sana kuimarika kwa maisha ya Watanzania.

Pambazuko tunaendelea kuwa na imani na uongozi wa Rais Samia katika kuwatumikia Watanzania na kuhakikisha neema inayopatikana kupitia kodi kutoka bandari na maeneo mengine, inagusa kila mmoja.

## ENDELEA KUPUMZIKA...



*Rais Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu Benjamin William Mkapa. Jumamosi iliyopita Septemba 16, rais alitembelea nyumbani kwa familia ya Mkapa Kata ya Lupaso, Masasi Mkoani Mtwara. (Picha na Ikulu).*

### Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### NUKUU



Kwa wale ambao bado mna wazazi wote au mmoja nasema; wapendeni sana sana. Waangalieni kwa jicho la pekee mno, hata kama wana “kausumbufu fulani.” Kumbuka, ipo siku hutasema naenda kumwona mama au mzee. Utaenda kutazama kaburi – Charles Misango (Mwandishi wa habari wa Tanzania).

## Tafakuri

## Matatizo yetu yanaanza kichwani

Na Thadei ole MUSHI

**E**THIOPIA ni nchi yenye idadi ya watu wanaoeleza kufikia milioni 117. Idadi hii ni mara mbili ya Watanzania wote kwa mujibu matokeo ya sensa ya mwaka huu – 2022 inayotaja kuwepo watu milioni 61.7.

Nchi hiyo ya pembe ya Afrika inapata zaidi ya dola za Marekani milioni 100 kila mwaka kwa kuuza umeme Kenya. Nchi hizo mwezi Oktoba, 2022 zilifunga mkataba wa kuuza na kununua umeme wa megawati 600 kwa miaka 25.

Chanzo kikubwa cha umeme huo ni maji ya Mto Nile ambao unaanzia Ziwa Victoria. Sehemu kubwa ya ziwa hilo iko Tanzania; kwamba asilimia 49 iko Tanzania, Kenya asilimia sita na Uganda asilimia 45.

Sambamba na hilo, Bwawa la Aswan kule Misri lina matumizi makubwa, ikiwamo hata kuzalisha umeme, chanzo cha maji yake ni kutoka Ziwa Victoria pia linahusika.

Iweje sasa Tanzania imelala tu na kushindwa kutumia maji hayo kuwa chanzo kikubwa cha umeme na shughuli zingine kubwa zenye kuleta mapato zaidi kwa nchi? Au kuna amri ya Mungu kwamba Tanzania itumie maji ya ziwa hilo kwa kuvua sato na sangara tu?

Sijui nani kairoga Tanzania, mbali na maji ya Ziwa Victoria kushindwa kutumika ipasavyo kupunguza umasikini, bado inashangaza nchi yetu kuwa na uhaba wa mafuta ya kula. Kila siku upungufu wa mafuta inakuwa ajenda ya kitaifa wakati tungeweza kuamua tu kuwa nayo mengi zaidi.

Haiieleweki kwanini Tanzania inashindwa kuwa kinara wa kuzalisha na kuuza mafuta ya kula zaidi ya Malaysia kwani hali ya hewa ya nchi hizo inafanana kabisa na kwamba nchi yetu ndiyo ilianza kulima zao hilo na wao



Ramani ya Tanzania

wakaja kujifunza na kuchukua mbegu. Wakatuacha “tumelala.”

Maajabu ya nchi hii ni mengi sana, mfano mwaka jana Uganda ilisaini mkataba wa kuuza maziwa ya ng'ombe nchini Zambia. Inafikirisha sana – kwamba Uganda na Tanzania ni nchi ipi iko jirani zaidi na Zambia? Kwa nini sisi tusingechukua ‘dili’ hilo la kuwauzia maziwa wakati tuna mifugo lukuki?

Baadaye nikagundua kuwa hata viwanda vyetu vya ndani havina uwezo wa kuuza maziwa ya kutosha , hivyo asilimia kubwa ya maziwa tunayotumia tunaagiza nje, hasa maziwa ya unga.

Uganda kwa mwaka wanazalisha maziwa lita bilioni 2.8; Kenya lita bilioni 3.43 huku Tanzania ikiwa inazalisha lita milioni 470 kwa mwaka. Ajabu sana!

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel alisema tatizo kubwa la nchi za Afrika siyo uhaba wa rasilmali, bali ni kutokuheshimu akili kubwa.

Makala haya yamerudiwa kwa sababu maalum; yalichapishwa mara ya kwanza ndani ya gazeti hili Desemba 10, mwaka jana - Mhariri

## **Ikulu yaisikiliza Pambazuko**

**Na Igo AI**

**K**ATIKA toleo lake nambari 46 la wiki kiliyopita, gazeti hili la wananchi; Pambazuko, liliandika habari ya kuitonya Ikulu ya Tanzania, kwamba tovuti yake rasmi ilibeba taarifa za uongo.

Kwamba ilibeba taarifa hizo kuhusu Baraza la Mawaziri la Tanzania, ambapo majina ya dhamana za baadhi ya mawaziri hayakuwa sahihi, ikiwamo nafasi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko.

Kwamba hadi alfajiri – Jumatatu, Septemba 11, saa 6:17 usiku, Tovuti Rasmi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilikuwa na makosa mengi.

Tovuti hiyo yenye anwani hii: [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz); ilikuwa ikionesha kwamba mawaziri walioabadilishwa ama kuondolewa kwenye baraza la mawaziri, bado wanahudumu kwenye nafasi zao za zamani.

Hatua hii ya kutobadilisha vyeo vya mawaziri ama kuwepo kwa walioachwa katika uteuzi wiki mbili zilizopita, ni makosa ambayo yalipaswa kurekebisha haraka.

Kutokana na taarifa ile ya Pambazuko, mapema asubuhi; Jumatatu ya Septemba 11; saa 4:22, watendaji wa Ikulu walisoma Pambazuko na hatimaye kurekebisha

makosa yaliyokuwa yakipaishwa na tovuti hiyo muhimu.

Watendaji wa Pambazuko, wakiongozwa na mhariri wake mkuu, wahariri, waandishi na hata wananchi wamepongeza Ikulu kwa kuwa sikivu na wepesi wake wa kurekebisha makosa.

Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Martha Mkina, alisema hatua ya Ikulu kusoma taarifa ya gazeti hili na kuchukua hatua, inapaswa kupongezwa na kwamba uharaka wa kutenda kazi unapaswa kuanzia hapo ili uigwe.

Baada ya mabadiliko hayo, sasa tovuti hiyo inaonyesha kuwa Dkt. Biteko ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Awali alionyesha kuwa ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini.


Tovuti hiyohiyo ambayo ilimtaja Dkt. Angeline Mabula kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakati aliondolewa katika nafasi hiyo. Sasa anatajwa waziri wake kuwa ni Jerry Silaa. Awali hakutajwa kabisa na picha yake haikuwepo.

Innocent Bashungwa, sasa anatajwa kuwa ni Waziri wa Ujenzi. Awali alitajwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kitu ambacho hakikuwa kweli.

Zaidi sana, tovuti hiyo ya ofisi nambari wahedi, inamtaja Prof. Makame Mbarawa kuwa waziri wa Uchukuzi. Awali alitajwa kuwa bado ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Jicho la Tai, ambayo ni safu mpya ya Pambazuko inajikita kurekebisha mahali ambapo kuna kulegalega kwa mambo ili hatua zichukuliwe.

Hongera Ikulu kwa kusoma Pambazuko na kuchukua hatua.



## Habari

## Nguvu ya AICC ukombozi wa uchumi

Na Tryruckia MFINANGA

**H**IVI karibuni, Tanzania ilielezwa kuhemewa na upungufu wa akiba ya dola za Marekani, hivyo kukwama kuagiza baadhi ya bidhaa muhimu kutoka nje, ikiwamo mafuta.

Hata hivyo, upungufu huo, unaweza kumalizwa na kuwa historia kwa nchi hiyo endapo serikali itawezeza na kutoa “baraka zaidi” kwa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kutekeleza mipango yake ya maendeleo, Pambazuko linaeleza.

“Kulialia” kwa serikali na sekta binafsi kuhusu upungufu wa dola za Marekani kunaweza kukoma ikiwa AICC; na taasisi zote zilizo chini yake, itapewa maeneo iliyoomba, kupewa na kuongezewa uwekezaji na zaidi sana rasilimali fedha.

Imebainika kuwa katika mabadiliko ya utendaji wa AICC, uongozi mpya chini ya Ephraim Mafuru, uwezekano wa kukusanya fedha nyingi za kigeni – kupitia utalii wa mikutano ya kimataifa, ni mkubwa zaidi.

Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa AICC, amesema makadirio yao ya mapato kwenye mwaka huu wa fedha (2023/24), ni zaidi ya dola milioni 48 za Marekani.

“Kiasi hicho cha fedha kitatokana na sisi kuandaa wastani wa mikutano 30 ya kimataifa katika mwaka huu wa fedha ambayo kila mmoja utahudhuriwa na wastani wa watu 1,000,” alisema Mafuru.

Mafuru aliyabainisha hayo katika mkutano na waandishi wa habari, ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina katika jitihada za kuonyesha utendaji wa tasisi za kibiashara za serikali zilizo chini ya ofisi hiyo.

“Na haya ni makadirio ya chini, tukijitahidi na kupata wastani wa wahudhuriaji 2,000 kwa kila mkutano, jambo ambalo tunaliweza, mapato hayo yataongezeka maradufu,” alibainisha.

Mafuru alisema kuwa utalii wa



Ephraim Mafuru

mikutano ni moja ya vyanzo vikubwa vya mapato ya fedha za kigeni barani Afrika na Tanzania ina nafasi kubwa ya “kufaidi keki” hiyo kwa sababu ina vigezo vingi vya kuvutia mikutano hiyo ukilinganisha na nchi ambazo zinaongoza hivi sasa.

Takwimu zilizotolewa hivi karibuni na ICCA; taasisi inayojihusisha na mikutano ya kimataifa, zinaonyesha kuwa hivi sasa Tanzania ni ya tano kuvutia mikutano mingi ya kimataifa Afrika ikitanguliwa na Afrika Kusini, Morocco, Rwanda na Misri.

Miaka mitano iliyopita Tanzania ilikuwa nafasi ya kumi kuvutia mikutano mingi ya kimataifa, huku ikimiliki asilimia tano tu ya soko ikilinganishwa na sasa ambapo inamiliki asilimia kumi.

“Ukiangalia baadhi ya nchi zilizotutangulia hazina vivutio vingi na vizuri kama ilivyo kwa Tanzania, wanachotushinda ni kutangaza kile kidogo walichonacho. Iwapo sisi wenye vivutio vingi zaidi tukiweka mkazo kwenye kujitangaza, ni dhahiri kuwa tutazipita nchi hizo kwa urahisi sana,” alisisitiza Mafuru.

Alisema kuwa na vivutio vizuri hakusaidii sana, bali kuvitangaza vivutio hivyo ndilo jambo litakalowavuta watu kuja nchini.

## **Nguvu ya AICC ukombozi wa uchumi**

*Inatoka Uk. 6*

### **Miradi mikubwa**

Mafuru, ambaye pia anasimamia uendesaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) kilichopo Dar es Salaam, alisema ili kujiimarisha zaidi, wamepanga kutekeleza miradi kadhaa mikubwa.

Alibainisha kuwa kuna mpango wa kujenga kituo kikubwa kitachojulikana kama Mount Kilimanjaro International Conference Centre (MK-ICC) ambacho kitakuwa cha kisasa zaidi na uwezo wa kuchukua wahudhuriaji wengi kwa wakati mmoja.

“Moja kati ya changamoto kubwa zinazotukabili hivi sasa ni kutokuwa na kumbi zenye uwezo wa kuchukua watu wengi kwa pamoja. Ukiangalia ukumbi wetu mkubwa wa AICC; Simba, una uwezo wa kuchukua watu kama 1,300 wakati ukumbi mkubwa hapa JNICC una uwezo wa watu 1,003.

“Hiki kituo kipya tunachopanga kukijenga, kitakuwa na ukumbi utakaokuwa na uwezo wa kuchukua watu 3,000 kwa pamoja. Pia tutatumia teknolojia ya kisasa itakayotuwzesha kuunganisha ukumbi huo na kumbi nyingine ili kuwawezesha watu katika kumbi nyingine kushiriki katika tukio linaloelelea kwenye ukumbi mkubwa,” alifafanua.

Alisema kituo hicho kipya na cha kisasa kitakuwa pia na hoteli za nyota tano na nyota nne pamoja na huduma nyingine muhimu ambazo watu wanahudhuria mikutano ya kimataifa watazihitaji.

Aidha, Mafuru alibainisha kuwa kuna miradi ya ukarabati mkubwa na upanuzi kwa ajili ya vituo vya AICC na JNICC ili kuongeza uwezo na ufanisi wake.

“Vivyo hivyo tutaangalia jinsi ya kuboresha rasilimali nyingine za kituo zikiwemo nyumba za kupangisha na hospitali, vitu tunavyovimiliki mkoani Arusha,” alisema.

Ili kuhakikisha kuwa shughuli zinazohusisha utalii wa mikutano zinakuwa na uratibu mzuri, Mafuru alisema wana mpango wa kuitisha mkutano mkubwa wa wadau wa sekta hiyo ili kupanga mikakati itakayowezesha kuifanya Tanzania kuvutia mikutano mikubwa na mingi ya kimataifa.

### **Madeni ni kikwazo**

Hata hivyo, pamoja na juhudi zinazofanywa na kituo hicho kuboresha utendaji, lakini madeni mengi, hasa wanayozidai taasisi za serikali, kimekuwa ni moja ya vikwazo vikubwa vinavyorudisha nyuma jitihada zao.

Alisema hesabu zinazonyesha kuwa wanazidai taasisi mbalimbali kiasi cha Sh. bilioni 7.4.

“Kati ya taasisi 20 tunazozidai, 17 ni taasisi za serikali ambazo deni lake kwa jumla ni asilimia 65 ya deni lote sawa na shiling bilioni 4.6,” alisema na kubainisha hata hivyo kuwa tayari wameshaanza mikakati ya kuhakikisha taasisi hizo zinalipa.

“Kama unazidai taasisi binafsi inakuwa ni rahisi kudai kwani unamwambia tu kuwa asipolipa deni lake, basi hawezi kupata huduma, lakini kwa taasisi za umma ni vigumu kidogo,” alisema.

Alitaja changamoto nyingine kubwa inayokikabili kituo kuwa ni uchakavu wa miundombinu kwenye kumbi za mikutano na nyumba inazozimiliki.

Mafuru aliyabainisha haya katika mkutano wa 14 wa taasisi za umma kuratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuonyesha utendaji wa taasisi za serikali ambazo shughuli zake zinahusisha utoaji wa huduma kibiashara.

Katika mikutano hiyo taasisi hizo zimeweza kuonyesha jinsi zinavyojiendesha kwa ufanisi wakati mwingine kushinda ufanisi wa taasisi binafsi.

## Tangazo

# Ukiwa Bukoba...

## Furahia Nene Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya;

|            |                   |
|------------|-------------------|
| Embe       | Nanasi/pinacolada |
| Passion    | Tende             |
| Parachichi | Tikiti            |
| Karoti     |                   |

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Waziliana nazi kwa  
namba hii:

**\*0753949488\***





## Kona ya Hoja

# Mchengerwa azibe matobo Tamisemi

Na Rashid Mtagaluka

**B**AADA ya kubaini kazi ya kunyoosha kivuli ni ngumu wakati uliopinda ni mti, Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ameona bora apande mti mwingine ili kupata kivuli nyooofu.

Ndivyo ninavyotafsiri hatua yake ya pangua-pangua ya baraza la mawaziri alioifanya hivi karibuni, ikiwa na lengo la kuongeza kasi ya utendaji serikalini.

Miongoni mwa mabadiliko aliyoyafanya Rais Samia ni kumpangia Mohamed Mchengerwa kuongoza Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi). Huyu alimuondoa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mchengerwa ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Rufiji mkoani Pwani, ni kati ya mawaziri wachache wa serikali ya awamu ya sita walioonesha kumudu vyema majukumu yao katika wizara wanazopangiwa.

Siyo siri na wala hakuhitajiki utafiti utakaochukua gharama kubwa kugundua kuwa wizara hii ya Tamisemi ndiyo wizara yenye 'makorokoro' mengi yanayowagusa wananchi wa kawaida moja kwa moja.

Hata hivyo inasikitisha kwamba idadi kubwa ya watendaji ndani ya Tamisemi, hasa wanaokutana na wananchi kwenye maeneo yao – uso kwa macho; watendaji wa vijiji, kata, wilaya na mikoa, wengi wamelala. Ni wazembe.

Inaelezwa kwamba asilimia 45 ya watu waliopewa dhamana ya kumwakilisha Rais Samia katika eneo la wilaya, hawafanyi kazi! 'Wanarilaksi' tu kwa msemu wa Mchengerwa.

Mchengerwa anasema amegundua kuharibika kwa mambo mengi na lawama kuangushiwa serikali kunatokana na kutokuchukuliwa kwa hatua pale

panapohitaji uamuzi wa haraka.

Anasema ubadhirifu mkubwa wa fedha, rushwa na vitendo vingi vichafu vikiwemo watu kutofanya kazi, ni matokeo ya watendaji kurilaksi."

Anasema kuwa taarifa anazo na kwamba sasa ameamua kutumia rungu la dhamana alionalo kurudisha Tamisemi kwenye mstari ili kuwa kimbilio la kila mwananchi.

Mchengerwa, anayeonekana kuwa kiongozi asiyetaka mchezo kwenye utendaji, anasisitiza kwamba hataki kusikia kuna mkuu wa wilaya yeyote nchini anashindwa kwenda kusikiliza na kutatua kero za wananchi kwa unyenyekevu.

Tayari waziri mwenyewe ameapa kutokaa ofisini, bali kufuatilia watendaji wote wa serikali walioko chini yake, mguu kwa mguu ili kuona wanawatumikia wananchi badala ya kuwa "mabwana wakubwa."

Nashauri kwamba ni vyema sasa Mchengerwa ajenge utamaduni wa wakuu wa wilaya na mikoa kuhakiisha wanajua vyema maeneo wanayoongoza, watu wake, maisha yao na zaidi sana kutambua kila miradi na kuisimamia kwa kila hatua ili kutatua kero za wananchi.

Ikiwa hakika waziri huyo anapenda kuona maendeleo na siyo kupiga siasa, basi kasi yake inaweza kuwa mwanga wa maendeleo zaidi kwa wananchi.

Pamoja na juhudi zake, ni vyema kila mmoja akasaidis maono ya Mchengerwa ili wakuu hao wa maeneo ya wilaya na mikoa, wafanye kazi na siyo kubaki viongozi wa kufungua na kufunga semina, kupokea mwenge, kuhudhuria mialiko ya mahafali tu.

• **Wasiliana nami kwa simu: 0784 438 546 au Email: mtagaluka@gmail.com.**

**Makala****WHO: Kunywa maji zaidi ni hatari**

Na Sylvia CHEBET  
TRT

**K**UNYWA maji kupita kiasi kunaweza kusababisha seli kadhaa za mwili kuvimba na kuvuruga utendaji wa ubongo, kunakoweza kusababisha mshtuko wa moyo, kukosa fahamu na hata kifo.

Mwanamke mmoja huko Marekani, Ashley Summers, mama wa watoto wawili, alikuwa likizo na familia yake katika Ziwa Freeman, Indiana mwezi Julai, mwaka huu, wakati akiwa huko alihisi kuishiwa maji mwilini, hivyo kuchukua chupa nne za maji – karibu lita mbili na kunywa haraka.

Baada ya muda mfupi mwanamke huyo alizimia. Familia yake ilimpeleka hospitali, lakini hakupata fahamu tena. Alifariki dunia.

Sababu ya kifo iliyoamuliwa na matibabu ilikuja kama mshtuko. Ashley, ilifahamika alikuwa alikufa kwa sababu ya “ulevi wa maji,” inayoletwa na kunywa maji mengi.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaeleza kuwa mamoja na umuhimu wa kunywa maji ya kutosha kila mara, lakini ni muhimu kupima na kuacha mazoea ya “kunywa hadi kuvimbiwa maji” kwani hatua hiyo ni hatari kwa afya ya binadamu.

Bruce Gordon, ofisa wa ngazi za juu wa WHO, akiwa mkuu wa kitengo cha maji na usafi wa mazingira, anasema watu wengi wamekuwa wakielezwa kuhusu faida za kunywa maji ya kutosha, lakini hawana ufahamu wa madhara ya kunywa maji mengi kupita kiasi.

Anaeleza kwamba maji ya ziada kupunguza elektroliti katika damu na kusababisha maji kuhamia ndani ya seli, na kuzifanya kuvimba. Hii inapotokea kwa seli za ubongo, inaweza kuwa hatari zaidi na hata kuhatarisha maisha.



Mtaalamu huyo wa afya anasema kwamba ndani ya mwili wa binadamu kuna aina ya madini ya sodiamu ambayo husaidia kudumisha usawa wa maji ndani na nje ya seli. Viwango vya sodiamu vinaposhuka kwa sababu ya matumizi ya maji kupita kiasi, baadhi ya viungo vya mwili hushindwa kufanya kazi.

Wataalamu wanasema dalili za maji kupita kiasi ni sawa na upungufu wa maji mwilini, na kuifanya iwe muhimu kwa binadamu kujipimia kiasi anachoweza kunywa kwa siku moja bila kusababisha madhara.

Mtu anayepungukiwa maji, kama ambaye amezidisha maji mwilini, wote wanaweza kuumwa kichwa, kuhisi kizunguzungu na kupata kichefuchefu; dalili ambazo ni za kawaida kwa hali zote mbili.

Inashauriwa kwamba binadamu hapaswi kunywa maji yanayozidi lita moja na nusu kwa saa.

“Kulingana na makadirio, hata katika hali mbaya ya kuwa na kiu kali, mtu wa kawaida hapaswi kunywa zaidi ya lita moja na nusu ya maji kwa saa,” anaongeza mtaalamu huyo kutoka WHO.

# Bukoba Raha

... Bukoba kuna senene  
... Bukoba kuna maji safi na salama

**Lakini Bukoba kuna G-smart Sauna & Steam Bath  
(Bafu la kuoga kwa mvuke).**

**Ukiwa Bukoba ama unaishi, usisahau  
kupata huduma G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Hakika hautajuta na ona fahari kusimulia  
wengine huduma za G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Faida za Sauna na Steam Bath ni nyingi,  
lakini chache ni zifuatazo:**

- Inaboresha afya ya moyo na mishipa
- Huondoa uchovu wa mwili na misuli
- Kuondoa msongo wa mawazo (stress)
- Kuzuia magojwa ya kukakamaa kwa misuli
- Inaboresha na kuhuisha mfumo wa usingizi
- Kuondoa sumu na kufanya ngozi nyororo zaidi

**Wasiliana na G-smart and Steam Bath  
walioko Barabara ya Kashozi na wapigie  
simu kwa namba: 0626 265725 / 0767 291 670**

**Habari****Tanzania yahofia vingi vifo NCD****Na Rashid Mtagaluka**

**O**NGEZEKO la idadi ya Watanzania wanaofariki dunia kutokana na magonjwa yasiyoambukizwa (NCD), inaendelea kupukutisha “nguvu kazi ya taifa,” hivyo kuitia hofu serikali.

Akiwasilisha mada katika kikao kazi kati ya Shirika la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANNCDA) na wahariri kilichofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Valeria Millinga alisema kwa hatua iliyofikia, jamii inapaswa kubadilika ili kuokoa nguvu kazi kubwa ya taifa.

“Nchini Tanzania asilimia 33 ya vifo vyote vinachangiwa na vifo vinavyotokana na magonjwa hayo ambayo yanaweza kuepukika, vyema sasa watu kubadili mfumo wa maisha,” anasema Millinga.

Shirika la Afya Duniani (WHO- 2016), linaeleza kuwa asilimia 75 ya vifo vyote duniani, vinavyohusu watu wenye miaka 30-70, husababishwa na magonjwa haya.

Akizungumzia mikakati ya serikali katika kukabiliana na changamoto hii inayoonekana kupunguza nguvu kazi kubwa ya Taifa, Millinga alisema ni pamoja na kuimarisha uratibu na mikakati ya kuzuia na kudhibiti kwa njia ya kuimarisha mfumo wa utoaji elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Mbali na mikakati hiyo, meneja huyo alisema kuongeza upatikanaji wa huduma za uchunguzi wa awali; hupatikanaji wa dawa na upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa Siko Seli.

“Upanuzi wa huduma za saratani kwa ajili ya kutoa huduma za mionzi kwenye hospitali zote za kanda na ujenzi wa Kituo cha Umahiri, Mloganzira na Dodoma pamoja na kuimarisha huduma katika hospitali za Mbeya, KCMC na Bugando, kutasaidia zaidi,” aliongeza.

**Valeria Millinga**

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Magonjwa Yasiyoambukiza, Dkt Omari Ubuguyu ameonya watu kuacha tabia ya kunywa pombe kupitiliza kwa maelezo kuwa kunachangia kwa kiasi kikubwa kasi ya magonjwa haya.

“Tanzania ni kati ya nchi zinazoongoza kwa unywaji pombe kwa wingi barani Afrika, kwani takwimu zinaonyesha kwa wastani, kila Mtanzania anatumia lita 9.1 ya pombe kwa mwaka sawa na ndoo ndogo ya maji”, alisema Dkt Ubuguyu.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa amevishauri vyombo vya habari nchini kurejesha vipindi vyenye maudhui ya kutoa elimu ya afya ili kuepuka ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza.

Msigwa ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye kikao kazi hicho alisema vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika kuelimisha jamii juu ya suala hilo na hasa ikiwa mashirika yaliyoandaa kikao kazi hicho yatatenga fungu kwa vyombo vya habari.

“Miaka ya nyuma Radio Tanzania ilikuwa na vipindi vilivyoishajihisha jamii kula chakula bora, hivyo hakuna ubaya iwapo vyombo vyenu vitarejesha vipindi hivyo ili kupunguza kasi ya magonjwa haya”, alisema Msigwa.

100% TRUSTED BRAND



# **DOR** **EASY WASH**

## **LIQUID SOAPS**

**USAFI WAKO  
NI JUKUMU LETU**

MANUFACTURED BY: DOR EASY WASH  
P.O BOX 80159 KIBADA, KIGAMBONI | DAR ES SALAAM - TANZANIA  
MOB: +255 715 771 123 | EMAIL: DOREASYWASH@GMAIL.COM

**Utalii****Afika kileleni K'njaro kwa saa 8****Na Nestory NESTORY**

**K**AWAIDA safari ya kupanda na kufika kilele cha mlima mrefu zaidi Afrika, Mlima Kilimanjaro huchukua siku tano hadi tisa.

Mlima huo wenye urefu wa mita 5,895 umeweka wastani huo na historia inaonyesha kwamba hakuna mtu aliyepanda na kufika kileleni chini ya muda huo wa siku tano.

Hata hivyo, mwanariadha wa Tanzania, Gaudance Lekule, ameishangaza dunia kwa kutumia saa nane tu, kupanda na kufika kwenye kilele cha mlima huo ulioko Mkoa wa Kilimanjaro.

Taarifa zinaeleza kuwa rekodi hiyo sasa imekuwa gumzo maeneo mengi ya dunia na tayari mwanariadha huyo ameanza kupata mialiko ya kutembelea nchi kadhaa za Ulaya na Amerika.

Akizungumzia siri ya mafanikio hayo, Lekule anasema kuwa mazoezi ndiyo nguzo kuu ya kufanikiwa kwake na kwamba kazi ya kupanda milima, siyo ngumu ikiwa mtu anayependa kufika kileleni kuweka nia ya kufanya hivyo.

Lekule ambaye ni mwanaharakati wa mazingira, anaeleza kwamba ameamua kutumia kipaji chake cha riadha kuutangaza Mlima Kilimanjaro duniani kote ili uweze kuvutia watalii wengi zaidi.

Anasema lengo jingine kubwa la kuhakikisha anavunja rekodi ya kutumia muda mfupi kufika kilele cha mlima huo ni kuhimiza kutunzwa kwa mazingira yanaouzunguka na pia kulinda barafu zake ili zisitoweke haraka.

“Kitu kingine kikubwa cha kupanda mlima huo ni kuleta hamasa kwa kila mtu; hata wasiopanda, ya kupata uelewa wa sababu za kupigania utunzaji wa mazingira ya mlima na pia kulinda barafu yake,” anaongeza.

Tafti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa eneo lililofunikwa kwa barafu kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro, limepungua kutoka kilomita za mraba 20 mwaka 1980 hadi chini ya kilomita mbili za mraba hivi sasa.

Inaelezwa na wataalamu wa mazingira kwamba kuyeyuka kwa kasi kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro kunatokana na kuwepo kwa ongezeko la joto, linalosababishwa na shughuli za binadamu katika maneo ya mlima huo, hasa kukata miti na kuchoma uoto wa asili.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Sayansi (Unesco) linaonya uharibifu wa mazingira katika maeneo yanayozunguka mlima huo kunaweza kusababisha barafu yote kutoweke ifikapo mwaka 2050.





# *Tangaza na* **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa  
huduma, endapo unahitaji kuwafikia  
wateja wengi zaidi bila kujali mipaka  
ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha  
na kupambazua huduma na  
biashara yako.

*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au  
Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

**Habari****Kashfa kubwa Jeshi la Polisi**

Na Mwandishi WETU

**M**AKUBWA yamefichuka! Ndiyo sentensi moja tu inayoweza kueleza tuhuma za kuwepo kwa baadhi ya maofisa wa ngazi za juu za Jeshi la Polisi Tanzania walivyokuwa wakipewa fedha bila kufanya kazi kupitia inayodaiwa kuwa akaunti ya mkuu wa chombo hicho cha usalama; IGP.

Taarifa zilizopatikana kwa gazeti hili la Pambazuko, zimeibuka ndani ya mahakama kutoka Jiji la London, Uingereza wiki iliyopita na habari zake kuchapishwa na vyombo vikubwa kadhaa duniani, ikiwamo gazeti lenye heshima zaidi Canada, The Globe & Mail.

Pambazuko limeona nakala kadhaa za barua-pepe zenye kueleza baadhi ya maofisa hao wa usalama kulipwa malipo ambapo yanabeba taswira inayodaiwa kuwa rushwa, kinyume cha sheria za utumishi, jeshi hilo pamoja na kampuni ya uchimbaji madini ya Acacia ambayo ndiyo ilikuwa ikitoa fedha hizo.

Acacia iliyokuwa ikiendesha shughuli za kuchimba madini kwa kumiliki migodi - ikiwamo ya dhahabu nchini Tanzania; North Mara, Tarime, mkoani Mara na Kahama Mining, Bulyanhulu, Kahama, Shinyanga.

Barua-pepe ambazo zimetolewa mahakamani zinaonyesha kwamba inayodaiwa kuwa akaunti ya IGP ilikuwa ikiingiziwa Sh. 20,000 kwa kila saa; kwa kila siku – saa 12, ikiwamo Jumamosi, Jumapili na hata siku za sikukuu kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Hiyo maana yake ni kwamba akaunti hiyo ya benki ya IGP ilikuwa ikipokea wastani wa Sh. milioni 21.6 kwa kila mwezi na endapo kiwango hicho kililipwa kwa mwaka, basi ilipokea Sh. milioni 259.2

Inadaiwa kwamba malipo haya kupitia akaunti ya IGP – ambayo namba yake haijatajwa, ni tofauti na gharama

ambazo kampuni hiyo ya madini ilikuwa ikilipa kwa serikali, kupitia Jeshi la Polisi, ikiwa askari wake walifanya kazi ya kulinda usalama migodini au maeneo yao ya kazi, nje ya migodi.

Pambazuko linazo taarifa kwamba askari wanaolinda kwenye maeneo ya biashara binafsi; kwa makubaliano maalum, hulipwa kati ya Sh. 20,000 na 30,000 kwa kufanya kazi kwa saa 12. Maeneo hayo binafsi ni pamoja na benki, shule na taasisi zingine.

Taarifa zaidi kupitia barua-pepe hizo na vyanzo vingine, ndani na nje ya mahakama hiyo, zinaeleza kwamba kwa kipindi cha miaka saba; 2008 hadi 2015, kulikuwepo kikosi kazi cha kulinda usalama wa migodi ya Acacia ambacho kilijumuisha maofisa kutoka idara mbalimbali za usalama.

Lengo kubwa la kikosi kazi hicho, ilikuwa kuhakikisha mali na wafanyakazi wa Acacia wanaishi na kufanya kazi kwa amani, bila hofu wala tashwishwi kutoka kwa ama wanaharakati, vibaka, majambazi na kila aina ya makundi ya uhalifu.

Katika kipindi hicho cha miaka saba, inadaiwa kwamba Acacia ilikuwa ikitumia zaidi ya Sh. bilioni tatu kwa mwaka kulipa maafisa kadhaa waandamizi wa serikali ya Tanzania. Hatua hii ilizua manung'uniko makubwa na hata “kuzaa” mgogoro wa ndani kwa ndani wa kampuni hiyo.

Baadhi ya maofisa wake walidai kwamba malipo hayo ya fedha kwa maofisa wa Tanzania yalikuwa yakipingana na sera ya “zuio la mazingira ya rushwa” na taratibu za uendeshaji wa kampuni hiyo na kuwa “haukufurahiwa na bodi yake hata kidogo.”

Imeelezwa kupitia barua-pepe za mawasiliano ya ndani ya Acacia Tanzania na uongozi wa juu; Canada na Uingereza, kwamba kikosi kazi maalum

## Kashfa kubwa Jeshi la Polisi

**Inatoka Uk. 16**

cha kulinda usalama wa kampuni hiyo kiliitwa Tanzanian National Law Enforcement Taskforce (NTF).

Polisi yakanusha

Pambazuko lilimtafuta Msemaji wa Jeshi la Polisi kuelezea kuhusu kashfa hii, lakini simu yake ya mkononi iliita tu bila majibu, na hata alipopelekewa ujumbe wa maandishi (meseji), hakujibu.

Gazeti hili lilimtafuta ofisa mmoja mwandamizi wa jeshi hilo, ambaye alikubali kuzungumza kwa sharti la kutotajwa jina kwani yeye hana mamlaka ya kufanya hivyo.

Alikiri kuwepo kwa utaratibu wa baadhi ya kampuni kuomba ulinzi wa Polisi na kwamba huingia makubaliano na wahusika hutakiwa kulipa.

Hata

hivyo, alikataa kuzungumza lolote kuhusu kuwepo kwa tuhuma za akaunti ya IGP kutumika kupitisha fedha za malipo ya askari kwa namna yoyote.

“Kama

kulikuwepo na utaratibu huo, basi ni jambo la ajabu sana, lakini kimsingi, ndani ya jeshi hakuna kitu cha namna hiyo, aliongeza.

**Kuibuka kwa kashfa**

Mara ya kwanza taarifa za kuwepo tuhuma za kulipwa mamilioni ya shilingi kwa NTF kuliibuka mwaka jana, 2022 baada ya kuanza kwa kesi ya kushitaki kampuni moja ya Uingereza ambayo ilitoa ithibati kwa dhahabu ya Tanzania kutoka Barrick Gold, kuuzwa nchini

humu.

Inaelezwa kwamba familia ya wanaharakati 10 walifungua kesi kupinga dhahabu hiyo kuuzwa kwa kile walichodai kuwa “inazalishwa kutoka eneo linalokiuka haki za binadamu.”

**Barrick Gold ndiyo iliyochukua umiliki wa Acacia.**

Tayari Barrick imekanusha kuhusika “kwa namna yoyote ile” na mwenendo wa malipo ya maofisa hao waandamizi wa Tanzania.

Katika taarifa yake iliyotolewa kwa umma Alhamisi iliyopita, Septemba 14, Barrick inaeleza kwamba inatambua kuwepo kwa kikosi kazi hicho cha maofisa wa usalama wa Tanzania na kwamba kazi zake kubwa ni kulinda usalama na kuhakikisha taifa hilo

la Afrika Mashariki linakuwa salama dhidi ya ugaidi na uhalifu mwingine mkubwa.

Barrick inadai kwamba Mei, 2014, Serikali ya Tanzania na Acacia ziliingia katika makubaliano

(MoU) ya kutumika kwa Jeshi la Polisi katika maeneo kadhaa ya ulinzi ili kuhakikisha usalama wa uwekezaji mkubwa wa Acacia.

Kampuni hiyo inaeleza kwamba malipo yote yaliyofanyika wakati huo yalikuwa halali na kwa mujibu wa taratibu ilizoita “halali” za serikali.

Inaendelea kueleza kwamba malipo yaliyanyika katika kipindi cha Mei, 2014 hadi Novemba, 2015 yalipokoma.

vering in...

...into Annexure A at item 6, presumably by Alfred Haonga. The ... is that the IGP is charging Tsh 20,000 per hour, for 12 hours of everyday, for ... including weekends and holidays, for each of our three mine sites, which come ...ly US\$10,000 per month. Do we have an understanding of this charge or what cost ...mbursing, or how this money will be used? It is apparently separate from the per diems ...taskforce officers which is covered in items 1 and 2 of Annexure A.

Many thanks  
Nick

6. Other incidental costs payable direct to the Inspector General's account are as follows

| S/N | DESCRIPTION                                | RATE                      | TOTAL              |
|-----|--------------------------------------------|---------------------------|--------------------|
| 1   | Charges per hour per Mining site           | Tshs 20,000/= x 1hr       | Tshs 20,000/=      |
| 2   | Contracted hours per month per mining site | 12hrs x 30 or 31 days     | 360 hrs or 372 hrs |
| 3   | Monthly charge per mining site             | Tshs 20,000/ x 360hrs     | Tshs 7,200,000/=   |
| 4   | Monthly charge per mining site             | Tshs 7,200,000/=x 3 sites | Tshs 21,600,000/=  |

From: M<sup>...</sup>  
Date:

## Riwaya

# Tetemeko la ndumba - 2

**Mtunzi:** Innocent N. ZAGALLO

“Tulia,” alimwambia. “Tulia. Usihofu, Mama Shaka.” Akauwasha msokoto wa tumbaku yake na kuvuta mikupuo miwili, mitatu kwa nguvu. Muda mfupi baadaye akapuliza moshi angani. Sasa akayarejesha macho kwa mkewe, Mama Shaka.

“Shaka amefungwa!” alisema kwa sauti nzito na ya chini sana akionyesha dhahiri kukumbwa na fadhaa.

“Nini?!” mkewe alitokwa macho pima. “Unasemaje Baba Shaka?”

“Shaka amefungwa!” Mzee Songoro aliirudia kauli yake, safari hii kwa msisitizo mkali.

“Nani kakwambia?”

“Hiyo hapo,” Mzee Songoro alisema huku akimwonesha mkewe kwenye televisheni. “Wametangaza sasa hivi na nimeiona picha yake kwa macho yangu haya!” akakielekeza kidole cha shahada usoni pake.

Mama Shaka alijikunja na kujikunjua pale sakafuni. Akahema kwa shida akiwa hayaamini masikio yake.

“Unaikumbuka ile kesi iliyokuwa ikimkabili?” Mzee Songoro alimuuliza.

“Ndiyo, naikumbuka.”

“Basi ni hiyo iliyomfunga.”

“Mungu wangu! Mwanangu Shaka!” Mama Shaka aliimboleza. “Mwanangu Shaka kafungwa! Kafungwa miaka mingapi?”

“Miaka mingapi?” Mzee Songoro alimtazama mkewe kwa namna ya kumshangaa. Kisha akaongeza, “Siyo wa

kutoka leo au kesho. Ni mpaka kiama!”

“Mungu wangu!” mkewe aliimboleza tena huku akitokwa machozi. Akajipigapiga kifuani kwa uchungu. Kisha akauliza, “Una maana kahukumiwa kifo?”

“Hakuna tofauti na kuhukumiwa kifo,” Mzee Songoro alijibu. “Hatutakaa naye tena hapa nyumbani tukizungumza. Kuonana kwetu ni mpaka twende gerezeni, na huko mtu unapewa dakika mbili, tatu tu za kuzungumza naye, tena askari akiwa kando yenu.”

Ulipita ukimya mfupi, wote wakiwa wamezama mawazoni. Mara Mzee Songoro akaibuka tena, na kwa msisitizo mkali akasema, “Mama Shaka, siwezi kumwacha mwanangu wa pekee afie jela. Kwa hilo siko tayari!”

Mkewe aliunyanuya uso na kumtazama, kisha akauliza, “Sasa utafanya nini Baba Shaka?”

“Nitajua la kufanya, lakini ni lazima nimwokoe mwanangu!”

\*\*\*\*\*

KILIKUWA ni kiapo cha Mzee Songoro, kiapo alichokitoa kwa dhati, kutoka moyoni mwake. Alfajiri ya siku iliyofuata aliamka na kutwaa kijimfuko kidogo, cheusi kisha akaondoka. Akachapa mguu hadi Mwembetogwa ambako alipata usafiri wa basi lililokuwa likielekea Kasulu. Yeye hakuwa na safari ya Kasulu, gari lilipokipita Kijiji cha Simbo na kwenda kilometa chache mbele, aliteremka.

Hapo alipoterekmia hakukuwa hata na nyumba wala dalili ya uhai wa binadamu. Kulikuwa na pori zito. Abiria wenzake, dereva na kondakta walimshangaa, lakini hawakumdadii kuhusu hilo.

## Kumbukizi

### Yanga yaomboleza Kigali



**Na Mwandishi WETU,  
Kigali**

**B**AADA ya kuifunga Timu ya Al Merrikh ya Sudan mabao 2-0 katika Uwanja wa Pele katika mchezo wa makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, juzi Jumamosi – Septemba 16, Yanga ya Tanzania jana ilipata wasaa wa kupita kwenye jumba la Makumbusho ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda, jijini Kigali.

Katika jumba hilo la makumbusho, viongozi wa Yanga, wachezaji na mashabiki walioongozana na mabingwa hao wa Tanzania, walisaini kitabu cha kumbukumbu na kila mmoja kusali kwa imani yake.

Mauaji ya kimbari ya Rwanda ya mwaka 1994, yanabaki kuwa kumbukumbu mbaya ya kuvugika kwa amani.

Watu wanaokadiriwa kufikia milioni moja walipoteza maisha katika mapigano ya wenyewe kwa wenyewe; makabila makubwa ya Wahutu na Watutsi.

Picha mbalimbali zinaonyesha Yanga wakiwa ndani na nje ya jumba na makumbusho hayo jana.

Tayari timu hiyo imefika Dar es Salaam na kwamba siku ya mwisho ya mwezi huu -Septemba 30, timu hizo zitacheza mchezo wao wa marudiano utakaochezwa jijini Dar es Salaam.

# MUNGU KWANZA...



**Ujumbe unaosambazwa kwenye magari makubwa, hasa nchini Tanzania umekuwa ukitumika kama darasa lisilokuwa na malipo kuelimisha umma. Gari hili linatangaza kwa kuhimiza watu kwamba hakuna mafanikio bila kumtegemea Mungu katika kila kinachofanywa na binadamu. (Picha na Mpigapicha Wetu aliyekuwa safarini Singida)**

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

